




JIJI LA GRAND RAPIDS

# SERA YA UTAWALA

NAMBAJI: 15-02	TAREHE: 23 Machi, 2015
SASISHO:	
IMETOLEWA NA: Meya wa Jiji	IMESAINIWA: 

**MAUDHUI: UCHUNGUZI WA AFISA WA IDARA YA POLISI YA GRAND RAPIDS**  
- ALIYEHUSISHWA NA UFYATUAJI RISASI

**DHUMUNI: KUWEKA UTARATIBU WA KUENDESHA UCHUNGUZI WA MATUKIO  
FULANI YA UTUMIZI WA NGUVU ISABABISHAYO MAUTI NA CHOMBO  
CHA NJE**

**SERA: UCHUNGUZI WA AFISA WA GRPD -ALIYEHUSISHWA NA UFYATUAJI  
RISASI VITENDO VYA KIHALIFU VITAREJELEWA KATIKA POLISI YA JIMBO LA  
MICHIGAN**

1. Kutokea kwa matukio arifu yafuatayo kutapelekea uchunguzi na uhusishwaji wa utaalamu wa kisayansi, usaidizi au ushirikiano wa MSP:
  - a. Mtu kupigwa risasi na afisa wa polisi wa Idara ya Polisi ya Grand Rapids katika utendaji kazi.
  - b. Kifo cha mtu yeyote kitokeacho akiwa chini ya uangalizi au ulinzi ama akiwa katika jaribio la kukamatwa na afisa yeyote wa GRPD.
2. Tukio arifu linapotokea, afisa wa GRPD aliyeopo eneo la tukio atachukua wajibu wa Afisa Kiongozi [OIC], kulingana na Taratibu za Muongozo wa GRPD 3-3; 7.1, 9-2.2-.5, hadi pale atakapoondolewa kwenye wajibu huo. OIC pamoja na maafisa wengine wa GRPD waliopo eneo la tukio watafuata itifaki na taratibu za ushughulikiaji wa OIS. Watakamata watuhumiwa wowote, watahakikisha kwamba watu wote walijeruhiwa wanapatiwa huduma za dharura za kiafya, na wataweka kingo za kulinda eneo la tukio ili kuzuia mtu asiyehusika kuingia kwenye eneo hilo.

3. Kisha OIC wa GRPD ataamuru mawasiliano yafanyike kwa Polisi wa Jimbo la Michigan na waombwe kuitika na kutumia rasilimali za MSP katika kuendesha uchunguzi wao. Kama MSP atashindwa kuitika kwa wakati na hali iliyopo ikawa ni ya dharura, basi OIC atakuwa na hiari ya kuchukua hatua mbadala inayohitajika kulinda watu wote na ushahidi wowote uliopo eneo la tukio.

4. Wakati wa kusubiria kufika kwa MSP, OIC na maafisa wa GRPD waliopo wataweka usalama kwenye eneo la tukio, watalinda na kuhifadhi ushahidi na nyaraka zozote zilizopo, na kutambua na kutenganisha mashahidi wowote walio polisi na walio wa kiraia, wakati wa kusubiria kufanyika kwa mahojiano ya awali. OIC atarekodi Taarifa ya Usalama wa Umma kutoka kwa kila afisa anayehusika kwenye tukio hilo na kisha atapanga maafisa wenzi wa kuwasindikiza kwenye eneo lililopangwa mbali na eneo la tukio.

5. Baada ya kufika kwa MSP, jithhada zote zitafanyika kuhakikisha usalama wa eneo la tukio kwa ajili ya wachunguzi wa MSP na wataalamu wa eneo la uhalifu. Wahudumu wa Afya na watenda kazi wa GRPD wataruhusiwa kuingia ndani ya mipaka ya eneo la tukio kwa kutegemeana na hali iliyopo. Watenda kazi husika wa MSP watachunguza tukio arifu hilo kwa kufuata taratibu za MSP. MSP ndio kitakachokuwa chombo kiongozi, kikishirikiana na Ofisi ya Waendesha Mashataka wa Jimbo la Kent.

6. GRPD itachunguza shughuli yoyote ya kihalifu inayohusika, iliyotangulia ama iliyotokea muda ule ule wa tukio arifu. Kamanda wa GRPD OIC pia atatoa usaidizi stahiki kwa MSP katika kipindi cha uchunguzi ufanyakao eneo la tukio. GRPD itaendesha uchunguzi wowote wa ndani ama ukaguzi wa kiutawala utakaohitajika kufanyika kufuatia tukio arifu husika. Hakuna nyaraka, ikiwa ni pamoja na ripoti za ndani, taarifa zilizopatikana kutoka kwa watenda kazi wa GRPD, ama taarifa yoyote ihusikanayo na hayo, itakayotolewa ama kupatiwa kwa wachunguzi wa uhalifu wa MSP.

7. MSP itashirikisha nakala za ripoti zote za uchunguzi kwa Ofisi ya Waendesha Mashtaka ya Jimbo la Kent na kwa GRPD kwa ajili ya mapitio.